

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mkoa wa Dodoma

Anwani ya Simu REGCOM
Simu Nambari: 2324343/2324384
E-Mail No. ras@dodoma.go.tz
Fax No. 255 026 2320046



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P 914,
Dodoma.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Jordan Rugimbana leo Julai 16, 2017 amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania - TIC Ndugu Geoffrey Mwambe na kukubaliana kuanzisha kituo cha pamoja cha Mfano cha kutolea huduma za uwekezaji (One Stop Center) Mkoani Dodoma, ambacho kitajumuisha taasisi zote muhimu zinazotoa huduma zinazohusiana na masuala ya uwekezaji na kukifanya kituo hiko kuwa na hadhi ya kanda ili kuhudumia mikoa yote iliyo jirani na Mkoa wa Dodoma kama Iringa, Singida, Tabora, Manyara na Morogoro.

Mheshimiwa Rugimbana amesema lengo la kuanzisha kituo hiko ni kuweka mfumo mzuri zaidi utaorahisisha utoaji huduma zote muhimu za kiuwekezaji kwenye eneo moja na kwa muda mfupi ili kuwaondolea usumbufu wawekezaji wanaokuja kuwekeza na kukumbana na changamoto na taratibu nyingi zisizo na umuhimu wowote.

"Hali ilivyosasa, wawekezaji wanakuja wengine wanaishia kwa Mkuu wa Mkoa, wengine Mkuu wa Wilaya, na wengine kwa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, pia matukio ya mara kwa mara ya kufunga shughuli mbalimbali na miradi ya uwekezaji kama viwanda yanababishwa na kutokuwa na mfumo mzuri wa pamoja wa kusimamia na kuwaelekeza wawekezaji juu ya masuala yote muhimu wanayotakiwa kuyafanya wanapotekeleza shughuli zao hapa nchini" alisema Mheshimiwa Rugimbana.

Katika kutekeleza azma ya Mheshimiwa Rais Magufuli ya kuifanya Tanzania kuwa ya viwanda, Mheshimiwa Rugimbana amemwelezea Mkurugenzi Mtendaji wa TIC kuwa tayari Mkoa wa Dodoma umeanza mchakato wa kutenga maeneo ya uwekezaji viwanda visivyopungua 100 kwa kila Wilaya vitakavyosimamiwa na Halmashauri za Wilaya na pia Maeneo ya viwanda visivyopungua 50 kwa kila Wilaya vitakavyosimamiwa na TIC kwa ajili ya wawekezaji wakubwa na wakigeni. Aidha, maeneo hayo lazima yawekewe miundombinu yote muhimu ya uwekezaji kama umeme, maji na barabara.

Nae Ndugu Geoffrey Mwambe amesema kuwa tayari TIC imeanza kuwaweka pamoja wadau wote wanaohusika na kusimamia masuala yanayohusu uwekezaji kama mazingira, Kodi, Usajili makampuni, Usalama mahala pa kazi, shirika la viwango na Uhamiaji kwa lengo la kuanzisha kituo cha pamoja.

Ameongeza kuwa wataweka mfumo wa kielektroniki utakaojumuisha mamlaka zote zinazosiamamia masuala ya uwekezaji na utoaji vibali mbalimbali hivyo wawekezaji watakuwa wanajisajili kielektroniki na lengo ni kupunguza zaidi usumbufu na muda wa kujisajili na kutoa vibali angalau usizidi siku tatu (3).

Amemalizia kwa kumweleza Mkuu wa Mkoa kuwa, TIC kwa sasa inajipanga kuongeza nguvu kwenvye eneo la utafiti wa masuala mbalimbali yanayohusiana na uwekezaji kama sera, mifumo, fursa za uwekezaji, maeneo ya Uwekezaji na changamoto mbalimbali zinazokabili sekta nzima ya uwekezaji hapa nchini.



Jeremiah Mwakwoma

Afisa Habari na Uhusiano

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dodoma

Julai 16` , 2017